

Juni 27, 2023

## Ujumbe kutoka kwa msimamizi wa shule zote, Ehren Jarret kwa wanafunzi, familia, wafanyakazi na wanajamii wote.

### *Mimi ni mzazi wa mwanafunzi wa RPS 205.*

*Hajjalishi umri gani au darasa gani, watoto wetu bado ni – watoto tu. Ni kazi yetu kama wazazi kuwalinda..*

Kama msimamizi mkuu wa shule zote, ni kazi yangu kuunga mkono walimu na wafanyakazi wetu katika kulinda usalama wa wanafunzi wetu shuleni kwa uwezo wetu wote. Ndiyo maana bodi ya shule ya RPS205 illiidhinisha usakinishaji wa vyombo vya kulinda usalama vya “**Evolve Express® security scanners**” kwenye milango kuu la shule zote nne za sekondari za RPS 205 – Auburn, East, Guilford and Jefferson, pamoja na shule ya Roosevelt. Vyombo hivyo vitasakinishwa na kutumika mwanzoni mwa mwaka wa shule wa 2023 – 2024 mnamo Agosti.

Vichanganuzi ambavyo vitakuwa milango kuu ya kuingiliya, vitaruhusu wanafunzi na wageni kutembea kwa urahisi kati ya vyombo hivyo bila kuondoa begi yao au kupunguza mwendo. Ingawa si vigunduzi vya chuma, **Vichanganuzi hivyo vinaweza kugundua vitu vya madhara mifukoni, koti na begi.** Lengo ni kutambua na kuondoa kila aina ya silaha na vifaa vingine vyenye madhara kabla ya vitu hivyo kuingia shuleni zetu. Kwa kuongeza, viingilio na njia za kutokea zenye usalama zaidi, zitaruhusu wanafunzi kupata uzoefu ya kibinafsi kama vile kuingia na kutoka katika mafunzo na miadi ingine kwa usalama.

Timu ya wataalamu wa sekta ya usalama pia walikamilisha tathmini ya usalama kwenye majengo ya shule yetu hivi majuzi, ili kubainisha maeneo ambayo tunaweza kuboresha. Kusanisha vichanganuzi vya usalama ni hatua moja tu tunachukua ili kufanya majengo yetu kuwa salama tuwezavyo kwa wanafunzi wetu, walimu na wafanyakazi ambao wanapaswa kujisikia salama katika mazingira yao ya majifunzo.

Kwa habari zaidi bonyeza kifute cha “**Learn More**” au ingia kwenye tovuti ya [rps205.com/evolv](https://rps205.com/evolv). Wakati wa mafungo hii ya kipwa, habari kuhusu na vichanganuzi au skana mpya zitapatikana kwenye tovuti ya wilaya, mitandao ya kijamii, na kutoka kwa wakuu wa shule za sekondari.

Kama wilaya ya shule, tunafanya kazi zetu na tunajitahidi kutumika na bidi ili kupata alama ya juu katika kuhakikisha shule zetu ziko salama kwa wanafunzi, familia, walimu na wafanyakazi.

**Asante kwa ushirikiano wetu katika kuhakikisha usalama na mafanikio ya wanafunzi.**

Dr. Ehren Jarrett  
Superintendent, Rockford Public Schools

(SWAHILI)